SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 2 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I2.4247

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# OMCHANGO WA METHALI ZA LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI KATIKA MALEZI NA MAKUZI YA WATOTO

Jina Saleh A. M. Saleh

Department of Languages and African Studies, Faculty of Languages, University of Sabha, Libya

**Keywords**:
Kimakunduchi
Lahaja
Methali
Mtoto
Jamii

**MUHTASARI**

Makala hii imechunguza mchango wa methali katika malezi na makuzi ya mtoto, methali hizo zimekusanywa kutoka kwenye lahaja ya Kimakunduchi kinachozungumza katika Wilaya ya kusini Unguja Zanzibar. Kwa kiwango kikubwa, methali za Wamakunduchi zimezoeleka kuonekana ndani ya vitabu kadhaa vya Kiswahili. Vitabu hivyo viwe vinahusu methali pekee, au hata vile vya hadithi na riwaya za Kiswahili. Katika makala hii, mtafiti amezigawa methali katika sehemu mbali mbali; kama vile:
'Asili/Historia ya jambo', utetezi wa matoto', 'Mahimizo ya kufanya ihsani', 'Methali zenye kufariji', 'Udogo wa mtoto' , 'Athari za mazingira' na mwisho mtafiti amechambua methali za jumla hazikumtaja mtoto wazi wazi.Baada ya mtafiti kuikamilisha kazi yake, amebaini kwamba methali za Wamakunduchi zina mchango mkubwa katika kumleza na kumkuza mtoto, na methali hizo zinasaidia kumwandaa mtoto kukua katika sura inayotakiwa na jamii. Mtafiti ametumia nadharia ya ' Ndani – Nnje' ambayo inasisitiza umuhimu wa kuujua utamaduni wa jamii ambayo mtafiti anataka kuihakikia kazi zake.

# مساهمة أمثال لهجة ماكوندوتشي في تربية وتنشئة الأطفال

صالح عبدالسلام محمد صالح

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية اللغات، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
ماكوندوتشي
لهجة
أمثال
أطفال
مجتمع

**الملخص**

إن الطفل هو نواة المجتمع ومستقبله، وحجر الأساس الذي تبني عليه الأمم حضارتها وتنميتها، ولأن مرحلة الطفولة تشكّل المرحلة الأكثر تأثيرًا على حياة الفرد، أضحى من واجب الأسرة والمجتمع والدولة توفير الحماية والرعاية والدعم اللازم لنمو الطفل وتنشئته على مبادئ المحبة والسلام، وتنمية قدراته ومواهبه. حيث تناولت هذه المقالة مساهمة الأمثال في تربية ونشأة الطفل، وقد جُمعت هذه الأمثال من لهجة "ماكوندوتشي" التي يتحدث بها في منطقة الجنوب بجزيرة أنغوجا في زنجبار. إلى حدٍّ كبير، اعتاد الناس رؤية أمثال قبيلة ماكوندوتشي في عدد من كتب اللغة السواحلية، سواء كانت هذه الكتب متخصصة في الأمثال فقط أو تتعلق بالقصص والروايات السواحلية. في هذه المقالة، قام الباحث بتقسيم الأمثال إلى عدة أقسام، مثل:
"أصل/تاريخ الشيء"، "الدفاع عن الطفل"، " الحثّ على الإحسان"، " أمثال المواساه"، " صِغر سن الطفل"، "تأثير البيئة."
وأخيرًا، تناول الباحث أمثالًا عامة لم تذكر الطفل بشكل صريح، وبعد أن أنهى الباحث عمله، توصّل إلى أن أمثال قبيلة ماكوندوتشي تسهم بشكل كبير في تربية الطفل وتنشئته، كما أنها تساعد في إعداد الطفل للنمو بالشكل الذي يريده ويقرّه المجتمع السواحيلي.

## Utangulizi

Fasihi simulizi ni urithi muhimu wa jamii nyingi barani Afrika, ikiwemo jamii ya Waswahili, ambao wamekuwa wakiihifadhi, kuieneza na kuitumia kwa vizazi vingi. Miongoni mwa vipengele vya fasihi hii ni methali – semi fupi zilizojaa hekima na maarifa yaliyokusanywa kutokana na uzoefu wa maisha ya jamii. Methali zimekuwa zikitumika kama chombo cha kuelimisha, kuburudisha, kuonya, na kuelekeza, hasa kwa watoto na vijana katika muktadha wa kijamii. Katika kisiwa cha Unguja, hususan eneo la Makunduchi lililo

*Corresponding author:
E-mail addresses: Sal.saleh@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 07 July 2025 - Received in revised form 10 August 2025 - Accepted 07 September 2025*

kusini mwa kisiwa hicho, methali hutumika kupitia lahaja ya Kimakunduchi – mojawapo ya lahaja kongwe za Kiswahili zenye asili ya kihistoria na utamaduni tajiri. Methali za Kimakunduchi si tu maneno ya busara, bali pia ni sauti ya mababu na mabibi wanaoendelea kuzungumza na jamii kupitia mafundisho yao ya maisha. Kwa muktadha wa malezi na makuzi ya watoto, methali hizi zimekuwa kama shule ya maadili, tabia, na hekima kabla hata ya kuwepo kwa elimu ya darasani. Malezi ya mtoto katika jamii ya Wamakunduchi yamejikita katika misingi ya kijadi, ambapo wazazi, wazee na jamii kwa ujumla hujihusisha kwa pamoja kuhakikisha mtoto analelewa kwa misingi ya maadili, heshima, nidhamu na utambulisho wa kitamaduni. Methali zimekuwa zikitumika kama nyenzo ya kufanikisha jukumu hili. Kwa mfano, kupitia methali, mtoto huonywa kuhusu hatari ya kutenda mabaya, hupewa motisha ya kuwa mchapakazi au mwadilifu, na wakati huo huo hujifunza kuhusu hulka na mila za jamii yake. Aidha, matumizi ya methali katika lugha ya asili (Kimakunduchi) huwasaidia watoto si tu kuelewa ujumbe unaotolewa, bali pia kuipenda na kuithamini lugha yao ya mama. Hii huimarisha uhusiano kati ya lugha, utamaduni, na malezi. Katika enzi ya mabadiliko ya kijamii na kisayansi, ambapo athari za utandawazi na lugha za kigeni zinazidi kushamiri, umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi methali hizi hauwezi kupuuzwa, kwani zinabeba misingi ya utambulisho wa jamii ya Wamakunduchi. Kwa msingi huo, utafiti huu au mjadala huu unakusudia kuchunguza kwa kina jinsi methali za lahaja ya Kimakunduchi zinavyochangia katika malezi na makuzi ya watoto – kwa maana ya maadili, tabia, maarifa ya kijamii, na ukuzaji wa utambulisho wa kitamaduni miongoni mwa kizazi kipya.

Katika kuielewa maana ya methali, tumewarejelea baadhi ya wataalamu ili tupate walivyotujuvya juu ya dhana hiyo. Wataalamu hao wametumiwa kama kigezo cha kutuongoza katika kuitambua dhana nzima ya methali na sifa zake. Mulokozi (2003) anaitambulisha methali kwamba ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na tajriba ya maisha ya jamii. Maana hii inatubainishia mambo matatu ya kimsingi. Kwanza, inatueleweshа taswira ya muundo wa methali, pili, ni sifa ya methali na ya tatu, kinachodhihiri ndani ya methali, kuwe na fikra au mafunzo mazito. Mauya (2008) anasema, 'Methali ni fungu la maneno yanayotumiwa pamoja kijamii kwa njia ya kufumba au kupiga mfano.' Ameendeleza maana hiyo kwa kusema, 'Methali ina maana pana kuliko maneno yenyewe yanavyotumiwa.' Maana hii (nayo) inatudhihirishia mambo mawili makuu. Kwanza, sifa ya methali (maneno ya kufumba), na ya pili, yale yanayojiri ndani ya methali hizo (zina maana pana – uzito). Said (2006) ameifafanua dhana ya methali kwamba, '… ni misemo, mafumbo, na kifungu cha maneno cha kisanii, chenye busara na maadili na kueleza kitu kwa picha ambamo ndani mwake mna tamaduni, desturi na hadhi ya jamii husika.' Tunapoitafakari maana hii tunadhihirikiwa na mambo kadhaa. Kwanza, sifa za methali (misemo au fumbo), pili, wasifu wake (kuwe na usanii/kuwe na taswira), na ya tatu, methali kama utambulisho wa jamii (huonesha tamaduni na desturi), na mwisho, yaliyomo ndani yake (kuna busara na maadili). Kwa kiwango kikubwa wataalamu hao wameweza kutuonesha njia tunayotaka kuifuata. Maana zilizotolewa zimesaidia katika utafiti huu hususan, katika kipindi cha ukusanyaji wa data. Maana hizo zilikuwa vigezo tosha vya kumuongoza mtafiti kukusaya methali badala ya nahau au vitendawili.

**Nadharia ya ( Ndani-Nnje )**

Hii ni nadharia mpya iliyoasisiwa na Tigiti S.Y.M.Sengo (1985 & 2009). Neno 'ndani-nnje' linaashiria umuhimu wa kuzingatia umbo la ndani na la nnje la kazi ya fasihi. Umbo la ndani ni msukumo wa nguvu za umbo la nnje la kazi husika. Kwa mfano, ndani ya 'chungwa' mnafahamika baada ya mtu kulimenya, kulikatakata, kulila, kuzikuta kokwa na vingine vya kuliwa ama kutupwa. Mjuzi huyo wa chungwa hatafanana na mshika chungwa, akaliona nnje tu, hajui ladha wala harufu. Kadhalika na jamii. Mpita njia na mkaazi hawashindani. Mwenye kuishi na watu wenyewe, watumiyao methali katika miktadha, mandhari, nyakati, marika, madhumuni na uhalisia kamili, atazifahamu methali hizo kwa undani kuliko wasomi waliopata kuropoka ati 'livundalo lina ubani', 'mvumilivu hula mbovu' na 'maji hayafuati mkondo.'

**Asili/Historia ya Jambo**

Inasadikiwa kuwa baadhi ya matukio huzuka kutokana na athari za urithi. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya methali zenye mwelekeo huo.

**Methali zenye Kuonesha Uasili wa Kitu**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Mwana ya nyoka naye nyoka | Mtoto wa nyoka naye ni nyoka |
| 2. | Mwana hufata kichogo cha mvyazi wakwe | Mtoto hufuata kisogo cha mlezi wake |
| 3. | Mwana wa haramu Hanakwaga | Mtoto wa haramu hajifichi |

Methali Na. 1 iimesawiri picha za nyoka, mzazi na mtoto wake. Methali zinaashiria wazo moja kuu; kwamba mtoto daima hufuata asili ya mzazi wake. Iwapo mama/baba ni Mwarabu, mtoto naye atabaki na sifa hiyo.

Methali Na. 1 ina mchango mkubwa. Zinamfumbua macho mwanadamu kuelewa kuwa asili ya mtu haipotei. Umuhimu wa kuelewa hivyo humzindua mtu kuwa makini na mwangalifu wa mtoto wake, yaani kama mzee wa mtoto alikuwa na tabia fulani iliyochukiza katika jamii, aghalabu ya mtoto naye hurithi na kuendeleza tabia hiyo. Jamii katika mwelekeo huu, hubaki na tahadhari kwa kila inapokuwa pamoja na mtoto huyo. Ingawaje kwa baadhi ya wakati hakuna usahihi wa jambo hilo.

Pamoja nazo, methali Na. 2 inakaribiana mno na mantiki ya methali iliyoitangulia. 'Kisogo', makaazi yake ni nyuma ya kichwa. Kwa kuwa kiko nyuma hubaki kama ishara ya tabia inayotarajiwa kufuatwa/kurithiwa na yule anayekiangalia. Hivyo, tunapoelezwa mtoto hufuata kisogo cha mzazi mlezi wake, tunapasa kutambua kwamba mtoto daima hurithi na kufuata tabia za mzazi wake. Hili hutufanya tuamini kwamba tabia za familia au jamii fulani hurithishana kizazi hadi kizazi. Huu ni msingi imara unaoyakinisha na kusadikisha kuwa mwenendo au utamaduni wa jamii fulani huendelezwa kwa miaka mingi na kuathiri kizazi kimoja na kingine.

Tunaweza kubaini mchango wake kuwa tabia za mtoto alizonazo ndizo alizorithi kwa wazazi wake. Mtoto ni kioo cha utambulishi wa tabia za familia yake. Hivyo hivyo, tabia za mtoto hubainisha wazi wazi malezi anayopewa na wazazi/familia yake.

Methali Na. 3 imetumia neno 'haramu' kwa maana ya mtoto aliyezaliwa nnje ya ndoa. Kwa uzoefu wa watu, mtoto wa aina hii aghalabu huwa na matendo yasiyoiridhisha jamii yake. Mara nyingi anakuwa mwovu na muharibifu wa mazingira. Hachelei aibu wala madhara ya anayoyatenda. Aidha, mtafiti alielezwa pia kuwa uharamu wa mtoto unaweza kutokea hata kwa mtoto mwenye kuzaliwa ndani ya ndoa. Alipoulizia kivipi, alielezwa kwamba iwapo chakula kilichopelekea kufanyika kwa tendo la ndoa kati ya baba na mama ni cha haramu, mtoto anaezaliwa naye hunasibishwa na sifa hiyo.

Methali hii inayo mchango wake. Ni chanzo cha kuelewa kwa watu juu ya mtoto husika. Iwapo ana tabia mbaya zisizokubalika katika jamii hasa za uzinzi na matusi, hufahamika kwamba asili ya mtoto huyo ni haramu. Mtoto halali daima hubaki na nidhamu njema. Kwa upande mwingine, methali hii hubaki kama karipio kwa mtoto mwenye tabia mbaya kwa hofu ya kuitwa mtoto wa haramu, na hivyo humfanya apunguze ukali wa maovu yake.

**Utetezi wa Mtoto**

Majawapo ya mambo muhimu ni suala la utetezi wa mtoto. Dini inamtetea mtoto na kutambulisha mambo muhimu anayostahili afanyiwe. Kwa mfano, kusomeshwa, kufunzwa utiifu na heshima, pamoja na kufunzwa maadili mema. Sekta nyinginezo za kidunia nazo zinahimiza suala hilo. Je, methali kama kipengele cha utamaduni wa Mswahili, zinaeleza nini juu ya jambo hilo. Tuchunguze methali hii:

**Methali zenye Kuonesha Utetezi wa Mtoto**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Mwana akanyea kiganja hakinakatwa | Mtoto akinyelea kiganja hakikatwi |

Methali Na.1 inaashiria utetezi wa mtoto. 'Kunya' katika mazingira yoyote yasiyokuwa chooni, huchukiza, seuze, kunyelea kiganja. Mtu hunya kinyesi. Kinyesi kinanuka, na ni uchafu usiofaa kuutizama licha ya kuwa karibu nao. Katika maendeleo ya kidunia, watoto wadogo

huvishwa kivazi maalumu chenye kuhifadhi uchafu wa kinyesi hicho. Anapomaliza kunya nguoni, kivazi hicho hutupwa jalalani. Je, iwapo atakunya kiganjani, kikatwe?

Ni dhahiri kwamba kinyesi katika methali hii kinaashiria maneno machafu au matendo maovu ya mtoto. Neno 'hakikatwi' linaashiria stahamala na subira mtu anayopata kuwa nayo pindi mtoto anapokosea. Mchango wa methali hii ni utetezi wa mtoto dhidi ya makosa yake. Yaani, si busara kutengana naye kwa vile amefanya kosa. Huo si ustaarabu, na ni kinyume cha msingi wa dini na mamlaka za kidunia. Hakuna asiye mkosa. Hii ni tahadhari kwa wazee wenye kiburi na hasira za papo kwa papo.

**Uhimizaji wa Kuwafanyia Watoto Ihsani**

Ihsani imesisitizwa sana katika imani za kidini na hata kwenye mila kadhaa za kidunia. Ni wema anaoufanya mtu kwa mwenzake. Kwa mfano, wema wa kumhurumia na kumtatulia shida zake, wema wa kukaa naye kwa vizuri, wema wa kumjali kuwa naye ni mwanadamu kama yeye, na wema wa kushauriana na kushirikiana naye. Tuzichunguze methali ifuatayo:-

**Methali zenye Kuhimiza Kuwafanyia watoto Ihsani**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Mwana ya mwenzio nae mwanao | Mtoto wa mwenzako naye ni wako |

Methali Na.1 inadhihirisha umuhimu wa kuwalea na kuwathamini watoto. Mtoto ni mtoto, anahitaji malezi ya kila mtu kwenye jamii. Hawezi kulelewa na wazazi pekee. Lazima jamii ishirikiane. Neno 'naye ni wako' lina maana nzito, linaonesha umilikishaji, yaani mtoto ni mali ya jamii.

Mchango mkubwa tunaoupata hapa kwamba wazee wawe wamoja katika kuwalea watoto. Waache tabia ya kila mtu kuwa na mwanawe/wanawe. Jamii yenye kushirikiana katika malezi hupata faida ya hifadhi ya heshima yao. Hivyo, watoto wanahitaji ihsani katika malezi yao.

**Kufariji**

Kufariji ni kuliwaza. Maliwazo humfanya mtu apate tahfifu ya yale yanayomsibu. Mgonjwa mathalani, au aliyefiliwa na damu yake, huhitaji kufarijiwa. Kwa baadhi ya wakati, faraja hupatikana kwa njia ya nasaha, ihsani, na wasia. Tuchunguze methali zifuatazo:

**Methali zenye Kufariji Watoto**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Mchawi mke mwana akulelee | Mchawi mpe mtoto alee |
| 2. | Teke la kuku halimuumizi mwanawe | Teke la kuku halimuumizi mtoto wake |

Methali Na. 1 inadhihirisha umuhimu wa hekima katika maisha. 'Mchawi' ni mtu katili na adui wa uhai wa mtu. Nguvu za mchawi ni kubwa na kutokana na usihiri wake anaweza kuingia ndani ya nyumba yoyote ilhali imekomewa. Mchawi hana mpenzi wala rafiki. Hana imani wala huruma. Kicheko chake ni kilio kwa wenzake. Fikra zake za kila siku ni juu ya nani atakaemsumbua usiku unaofuatia.

Methali hii imetawaliwa na hekima kubwa. Yaani, kama kuna wasiwasi juu ya uadui wa mtu fulani dhidi ya kitu fuani, ni busara kwa mtu huyo kumkabidhi kitu hicho. Kwa mfano, iwapo bibi ni mchawi anaetiliwa shaka ya hujuma kwa watoto, ni vyema mtoto huyo apewe yeye kwa lengo la kumlea. Yasadikiwa kuwa hawezi kumdhuru ila atamlinda.

Methali Na. 2 inabainisha hadhari iliyopo ya mzee kwa mtoto. Neno 'teke' ni kitu cha hatari kinachoweza kusababisha hata mauti. Kiumbe chochote kinapopigwa teke hakiachi kuathirika. Ingawa hivyo, teke la methali hii halina madhara yoyote. Hii inadhihirisha hadhari inayochukuliwa na mzazi wakati wa teke hilo.

Methali inao mchango. Inajaribu kuwafariji watoto kwamba hakuna mzee mwenye uadui na mtoto wake. Daima mzee yuko mstari wa mbele katika kumhami mwanawe. 'Teke' kwa upande mwingine linaashiria adabu/adhabu anayoitoa mzazi kwa mtoto kwamba daima huwa na 'mpaka'.

**Udogo wa Mtoto**

Katika kuendeleza malezi yaliyo bora, ziko baadhi ya methali zenye kuonesha hisia za udogo wa mtoto kwa mzazi. Kwamba kadiri ya mtoto/mtu anavyokuwa bado aelewe kuwa akiwa mbele ya mzazi wake, hubaki mtoto.

**Methali yenye Kuonesha Udogo wa Mtoto**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| 1. | mwana hanakuwa<br>Kwa wavyazi wake | mtoto hakui<br>kwa wazazi wake |

Methali Na.1 inadhihirisha hekima, busara na utiifu wa mtoto anaotakiwa awe nao kwa wazazi. Methali haina maana ya mtoto mdogo peke yake, bali inamzungumzia binadamu katika hatua zote za maisha - kiumri, kihadhi, kielimu, na mengineyo. Mtoto mbele ya mzazi ni mtoto, hata awe na mvi. Mchango mkubwa unaobainika hapa kwamba mtoto achunge heshima ya wazazi katika maisha yake yote. Elimu, mali, rika au cheo si jambo lenye kupunguza hadhi na utukufu wa mzazi. Mzazi ni mzazi hata awe mjinga au mpumbavu.

**Athari za Mazingira**

Dhana ya mazingira imekuwa ikizungumzwa katika maeneo mbali mbali kama mikutanoni, vitabuni, magazetini, mashuleni, maofisini, na kwenye vyombo vya habari kama redio na televisheni. Leo hii kuna wizara maalumu yenye kushughulikia suala la mazingira. Utamaduni wa Mswahili nao unayafafanua mazingira na athari zake. Hebu tuichunguze methali ifuatayo na jinsi inavyoelezea taathira ya mazingira kwa mtoto.

**Methali yenye Kuonesha Jinsi Mazingira Yanavyoathiri**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Mwana ya kima hanafundwa Kulya ukwaju | Mtoto wa kima hafundishwi kula ukwaju |

Methali Na.1 inadhihirisha jinsi mazingira yanavyoathiri. Mtoto amekuwa na tabia ya kujifunza matendo kadhaa kwa njia ya wigo. Inakadiriwa kuwa matendo mengi anayoyafanya hutokana na wigo kuliko kufunzwa kutoka kwa mzazi. Methali imemtaja mtoto wa kima kama ni taashira ya mtoto wa kiumbe chochote. Iwapo mwana wa kima hafunzwi kula ukwaju, ni dhahiri kuwa yule wa binadamu hatafunzwa maradufu.

Methali inampunguzia mzazi wajibu wa kumfunza mwana. Asiwe na wasiwasi. Aelewe kuwa licha ya mafunzo kutoka kwao, mazingira nayo yana nafasi yake. Hii ndiyo inayomlazimu mtoto kufanya mengi anayoyafanya bila ya kueleweshwa na wazazi wake. Kwa upande mwingine, methali inamuonya mtoto kutobaki bila kujifunza kwa kusubiri kufunzwa na mzazi. Ana wajibu wa kuangalia mambo jinsi watu wanavyoyafanya, na yeye ayafanye.

**Methali za Jumla**

Aina nyingine ya methali ni za jumla. Kifani, hazikumtaja mtoto wazi wazi. Kinachojitokeza ni lugha yenye kuashiria uhusika wa mtoto. Methali hizo zimeorodheshwa ndani ya jadweli lifuatalo.

**Methali za Jumla**

| Na. | Kimakunduchi | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| 1. | Ukalembea bwe kundini kuchaumiza yako | Ukirusha jiwe kundini utaumiza wa kwako |
| 2. | Kuwa uyone | Kuwa uyaone |
| 3. | Mkamia maji hayanywi | Mkamia maji hayanywi |
| 4. | Bora kujikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi | Bora kujikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi |
| 5. | Njia ya mwongo fupi | Njia ya mwongo ni fupi |
| 6. | Siku za mwivi arubaini | Siku za mwizi ni arubaini |
| 7. | Mkaidi hafwaidi mpaka siku ya Iddi | Mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Ukupigao njo ukufundao | Ukupigao ndiyo ukufunzao |
| 9. | Hakuna dume pweke | Hakuna dume pekee |
| 10. | Mnatembea na mwivi nae mwivi | Mtembea na mwizi nae ni mwizi |
| 11. | Hasidi hana rafiki | Hasidi hana rafiki |
| 12. | Mnavua nguo huchuchama | Mwenye kuvua nguo huchutama |
| 13. | Usimwage mtama vanavo kuku wengi. | Usimwage mtama kwenye kuku wengi |
| 14. | Mcheka kilema hafu hajachona | Mcheka kilema hafi mpaka kimpate |
| 15. | Mkamatwa na ngozi njo mwivi | Mkamatwa na ngozi ndiye mwizi |

Methali Na.1 inawaasa wazee kuacha tabia ya kulenga jiwe kwenye kundi la watu. Jiwe ni taashira yenye kuwakilisha jambo/kitu chochote chenye kusababisha hatari. Mfano, silaha na hata kauli zenye uadui. Iwapo mzazi anatoa kauli mbaya au shutuma nzito katika kikundi ambacho ndani yake yumo anaemuhusu, yamkinika madhara yake yakamsibu aliye wake. Hivyo, methali hiyo licha ya nasaha hizo, kwa upande mwengine imebeba dhima ya kumtetea mtoto.
Methali Na.2 ni tanbihi kwa watoto. Waache tabia mbaya walizonazo kama za kuupuzia wanavyoelekezwa na wazazi wao. Neno 'kuwa' lina maana ya utu uzima, ilhali 'uyaone' linadhihirisha hamu ya mzee ya kumuona mtoto wake amekuwa mkubwa. Hamu hiyo haiashirii heri, bali kwa kiwango kikubwa huashiria shari. 'Akuwe ayaone' kwa maana 'akuwe' ili naye yamkute kama yanavyomkuta mzee wake.
Methali Na.3 inaendeleza tanbihi kwa watoto. Yaani, wasiwe na pupa katika jambo lolote. Aghalabu ya pupa haina mwisho mwema. Nayo methali Na.4 ina mchango kwa mtoto. Inamlea awe na tabia ya kujiepusha kusema maneno yasiyo kaida wala nidhamu. Neno linaposemwa huwa limeshasemwa, haliwezi kusahaulika. Hivyo, methali inawaasa watoto wawe na nidhamu ya kuongea.
Methali Na.5 – 6 zina mwelekeo wa aina moja. Zote ni makatazo kwa mtoto kwamba aache tabia mbaya kama ya kusema uongo na kuiba. Hivyo, methali hizo zinamuasa mtoto awe na tabia njema.
Methali Na.7 nayo inaendeleza nasaha kwa mtoto. Asiwe na tabia ya ukaidi. Yaani, aepukane na tabia ya kupinga jambo lililo ndilo, hususan neno au jambo lilotolewa na mzee. Nasaha zote zimo katika azma ya kumlea mtoto ili aishi maisha bora katika jamii.
Methali nyinginezo zilizobakia zimo katika utaratibu wa kumlea na kumkuza mtoto ili awe ni mfano mwema kwa jamii. Kwa mfano, methali Na.8 inamwelekeza mtoto ayakabili matatizo yanayompata kama funzo la kuepukana nayo pale yanapojitokeza tena. Methali Na.9 inawaonya watoto waache tabia ya kujitukuza na kujihisi kuwa ni bora zaidi, ilhali, wapo wenye kuwazidi. Methali Na.10 inamtaka mtoto aepukane kushirikiana na vikundi viovu ili asije akashabihishwa navyo. Methali Na.11 inaafikiana na Na.10 kwa kumtaka mtoto asifungamane na watu waovu. Methali Na.12 inawahimiza watoto pale wanapopata shida wakubaliane na matokeo. Yaani, wazikabili shida hizo kwa moyo mkunjufu ili wasitirike na aibu mbali mbali. Methali Na.13 ni fundisho kwa mtoto kuwa aweze kuficha siri, na pia asiwe na haraka ya kueleza jambo zito mbele ya kila mtu.
Methali Na.14 ni hadhari kwa watoto. Waache tabia ya kucheka ama kufanya stihizai kwa walemavu kwa upande mmoja, pia kwa upande mwingine, waelewe kuwa kila linalompata mwenzake, upo pia uwezakano wa kumpata yeye. Methali Na.15 inakubaliana na Na.

**Hitimisho**

Methali za Wamakunduchi ni urithi mkubwa wa fasihi simulizi unaochangia sana katika malezi ya mtoto. Zinajenga maadili, zinatoa mwongozo wa maisha, na zinathibitisha kuwa jamii ni mshiriki mkuu wa makuzi ya mtoto. Methali hizi zinaweza kuwa mbadala mzuri wa adhabu kali, kwa kuwa zinajenga kwa busara na maarifa ya jamii. Muhimu kwa jamii za leo kuzihuisha methali hizi kwa kuzifundisha mashuleni, kuzitumia katika mawasiliano ya kila siku, na kuzihifadhi kama hazina ya maarifa ya malezi.

**MAREJEO**

1. Akaka, L. & Wandera-Simwa, S. (2024) Iktibasi katika Methali za Waswahili
Journal of Kiswahili, UDSM, Vol. 86 (2).
2. Alexander, C. 2004 "Matumizi ya Methali na Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii". Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).
3. BAKITA ( 2012 ) Kamusi la lahaja ya Kimakunduchi. Jamana Printers Ltd. Toleo la Kwanza.
4. Jared, N. 2004 "Methali na Suala la Umri: Matumizi ya Methali katika Jamii Mifano Kutoka Rika Mbali mbali za Wanyambo". Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).
5. Kunemah, A. 2009 *Misemo na Methali katika Ushairi*. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
6. Mauya, A 2008 Semi: Maana na Matumizi. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
7. Murithi, M. M. (2015) Uchanganuzi wa methali za Kiswahili: mtazamo wa kiudenguzi. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta.
8. Sengo, T. S.Y. M. 2009 *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam. AERA KISWAHILI RESEARCH PRODUCTS